

# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1

Fax Nam. + 255 24 2230215

Tovuti: [www.zanzibarassembly.go.tz](http://www.zanzibarassembly.go.tz)



SANDUKU LA BARUA 902,

ZANZIBAR

Barua Pepe: [zahore@zanlink.com](mailto:zahore@zanlink.com)

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

### TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA SITA WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR AMBAO UTAJADILI BAJETI YA SERIKALI UTAKAOANZA TAREHE 10 MEI, 2017.

Mkutano wa Sita wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 10 Mei, 2017, saa 3:00 asubuhi.

#### **SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA.**

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

#### **1. Maswali na Majibu.**

Maswali 182 yameratibiwa kwa ajili ya kujibiwa kwenye Mkutano huu.

#### **2. Majadiliano ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018.**

#### **3. Miswada ya Sheria**

**Miswada ya Sheria itawasilishwa na kujadiliwa, Miswada yenyewe ni:-**

- i. Mswada wa Sheria ya Fedha (Finance Bill)
- ii. Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018.
- iii. Mswada wa Sheria ya (Marekebisho) ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015.

#### **Miswada ya Dharura**

- iv. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ushuru wa Stempu (Stamp Duty) na kuwekwa Sheria Mpya ya Ushuru wa Stempu.
- v. Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa (Exercise Duty)

#### **4. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka 2014/2015.**

#### **5. Taarira za Serikali Kuhusu Utekelezaji wa Hoja.**

- i) Taarifa ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Uingizaji na Utumiaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar, na

- ii) Taarifa ya Wizara ya Uwezesaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Hoja ya Baraza la Wawakilishi kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Kisheria na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

**6. Mswada kusoma kwa mara ya kwanza ambayo Serikali italeta kabla ya kuahirishwa kwa Mkutano huu wa Baraza.**

**(Raya Issa Msellem)  
Katibu  
Baraza la Wawakilishi  
Zanzibar**

**8 Mei, 2017**